# KATIBA

# YA

# TANZANIA LAYERS FARMERS ASSOCIATION

# (TALFA)

TALFA

# 2017

VIFUPISHO, TANBIHI NA LUGHA

1. VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **TALFA** | **TANZANIA LAYERS FARMERS ASSOCIATION** |
| S.L.P.- | SANDUKU LA POSTA |

2. TANBIHI;

1) Katika katiba hii, Neno chama litakuwa na maana iliyosawa na neno Umoja au kikundi.

2) Katika katiba hii, Neno Mwanachama litakuwa na maana iliyosawa na neno Mwana-Umoja au Mwana-kikundi

3) Neno Madhumuni litakuwa sawa na Malengo

3. LUGHA;
Lugha itakayotumika itakuwa ni Kiswahili na Kiingereza

TALFA

## TAFSIRI

Kwa madhumuni ya Katiba hii na taratibu zitakazotengenezwa chini yake masharti yafuatayo, maneno, misemo na majina yafuatayo yatatumika kama ifuatavyo:

a) **Chama:** Tanzania Layers Farmers Association(TALFA)
b) **Katiba:** Maana yake ni Katiba yaTanzania Layers Farmers Association(TALFA)
c) **TALFA:** Ni kifupi cha Tanzania Layers Farmers Association
d) **Kamati ya Utendaji:** Maana yake ni kamati iliyochaguliwa kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa kuendesha na kuangalia mwenendo na shughuli za Chama.
e) **Mkutano Mkuu wa Mwaka** : Maana yake ni mkutano wa wanachama wote utakaoitishwa na kufanyika mara moja kwa mwaka kujadili shughuli za Chama
f) **Wanachama:** Maana yake ni Waanzilishi, wa Kawaida, Washirika, Mwanachama wa Heshima wa Chama
g) **Mwaka wa Fedha:** Mwaka wa fedha wa Chama utaanza tarehe 1Januari mpaka 31 Desemba ya kila mwaka
h) **Kanuni:** Maana yake ni kanuni zilizotengenezwa au zitakazotengenezwa chini ya sehemu ya Saba (7) ya Katiba hii

TALFA

## UTANGULIZI

**KWA KUWA,** sisi wanachama wa Tanzania Layers Farmers Association (TALFA) tumeamua rasmi na kwa dhati kuunda na kujenga hiki kikundi kwa hiari kwa lengo la kufanya shughuli za kiuchumina kijamii kwa ustawi wa wanachama wake. Kikundi hiki kimeanzishwa rasmi tarehe **12.9.2016**

**NA KWA KUWA,** kwa pamoja wanachama wanaahidi kuilinda na kuitekeleza katiba hii. Pamoja na Katiba hii, kikundi hiki kitaendeshwa kwa mujibu wa kanuni mbalimbali ambazo zitawekwa na wanachama.

**HIVYO BASI, KATIBA HII YA TANZANIA LAYERS FARMERS ASSOCIATION,** imetungwa na **SISI WANACHAMA WA TANZANIA LAYERS FARMERS ASSOCIATION** kupitia kikao cha wanachama kwa madhumuni ya kusaidiana sisi wanachama wa Tanzania Layers Farmers Association katika shughuli za ufugaji wa kuku wa mayayi.

TALFA

**IBARA YA 1: JINA NA ANUANI, OFISI NA MAKAO MAKUU NA ENEO LA KIUTENDAJI LA KIKUNDI**

a) **Jina la Kikundi**

1. Jina la kikundi hiki litakuwa "TANZANIA LAYERS FARMERS ASSOCIATION (TAFLA)"

b) **Anwani**

TANZANIA LAYERS FARMERS ASSOCIATION (TAFLA)

S.L.P 77734

DAR ES SALAAM

c) **Ofisi**

Chama kitakuwa na ofisi yake katika jengo la Platinum International Agency Ltd Old Bagamoyo Road Plot No. 799 Mikocheni.

d) **Makao makuu**

Chama kitakuwa na makao yake ya muda katika jingo la Platinum International Agency Ltd Old Bagamoyo Road Plot No. 799 Mikocheni.

e) **Eneo la Utendaji kazi**

Eneo la Utendaji kazi litakuwa eneo la nchi ya Tanzania ambapo chama kitanzisha matawi yake.

**IBARA YA 2 : Madhumini**

Tanzania Layers Farmers Association (TAFLA) ni kikundi kisicho kuwa cha siasa, kikabila wala kidini bali ni Kikundi kinacho shughulika wanachama wake kina malengo yafuatayo;

TAFLA

a) Kutambuana na kuzungumza kwa njia ya kuleta uhusiano mwema miongoni mwa Wanakikundi;

b) Kuhamasishana miongoni mwa Wanakikundi kutoa michango mbali mbali ya kuimarisha Kikundi;

c) Kusaidiana katika masuala ya kijamii wakati wa shida na raha hasa kwenye mazishi, harusi na maradhi;

d) Kuwa jukwaa kwa chama cha Tanzania Layers Farmers Association. Kuibua maswala, kujadili na kutafuta ufumbuzi wa pamoja kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine muhimu.

**e)** Kuanzisha na kudumisha taasisi katika Tanzania kwa ajili ya kukuza maendeleo na mwongozo wa biashara katika sekta ya mayai kama taasisi tanzu inayojitegemea katika tawi la chama cha Poutry Association of Tanzania (PAT) kwa kuwa na hadhi sawa kama zinazopewa tanzu nyingine ambazo ni matawi ya sekta ya kuku.

**f)** Kuwa nguvu ya pamoja kwa ajili ya kujadiliana, kuzungumza, kuanzisha, kuchunguza na kutoa ushauri kwa maswala makubwa yanayogusa maslahi ya wanachama kwa pamoja au mmoja mmoja.

**g)** Kuwakilisha wanachama katika majadiliano na serikali, na umma na taasisi zisizo za kiserikali kwa maslahi mapana ya wanachama.

**h)** Pale nafasi itakaporuhusu, kuwaelimisha wafugaji wa kuku wa mayai njia za kisasa za ufugaji wa kuku kwa kutengeneza mazingira mazuri. Kuhamasisha elimu ya ufugaji kwa kufanya au kusaidia katika uchunguzi wenye asili ya kinadharia na kisayansi na kuandaa warsha kwa kuanzisha na kuongeza utamaduni wa kujifunza miongoni mwa wanachama wa TALFA.

**i)** Kujenga uhusiano na watunga sera, mashamba mama ya kuku wazazi, watengenezaji wa chakula, wasindikaji wa bidhaa za kuku na masoko kwa lengo la kuongeza uzalishaji.

**j)** Kuhakiki kwa umakini usalama wa kuku na mazao kwa kutembelea mifugo ya wanachama.

**k)** Kulinda haki ya walaji dhidi ya bidhaa dhaifu za kuku na mazao yake.

TALFA

**l)** Kupeana mbinu miongoni mwa wanachama kuinua uchumi wetu.

**m)** Kupeana mbinu bora za ufugaji miongoni mwa wanachama.

**n)** Kutetea ili kupata hali bora katika shughuli zinazo athiri uchumi na ustawi wa wanachama.

**o)** Kuhamasisha utafiti na maendeleo ya mfumo wa uzalishaji wa kuku ndani ya nchi miongoni ya mwanachama.

**p)** Kuratibu ushirikiano na mashirika mengine ya kimataifa katika kuleta maendeleo ya sekta ya kuku kwa faida ya wanachama.

**q)** Tathmini jadidi ya mbinu ya kudhibiti miundo ya uboreshaji katika sekta, inaweza kupimwa kwa kuongezeka kwa matumizi ya mayai nchini Tanzania.

**r)** Kujenga uhamasishaji wa bidhaa kwa kukuza soko kwa ajili ya sekta ya mayai kupitia mafanikio ya kampeni ya **"Eggs are magic"**

**s)** Kushughulikia jambo linguine lolote ambalo litakuwa ni kwa maslahi mapana ya sekta, Chama na wanachama wake.

**t)** Kuwezesha, kushawishi na kuwasiliana na serikali na wakala wa serikali kuhusu ubora na hatma ya kuendeleza wafugaji wadogo na wakulima kwa kuwahakikishia ufanisi unaofaa katika hali ya utoaji wa msaada katika kila eneo.

**u)** Kupeana elimu inayohusu maendeleo katika sekta ya kuku miongoni mwa wanachama.

**v)** Kukusanya taarifa za soko na kuzifanya zipatikane kwa wanachama wote wa TALFA kwa kuwasaidia kufanikisha bidhaa zao sokoni na uelewa wa ugavi kwa ujumla.

w) Kuwa na mikakati ya maendeleo ya soko itakayoleta tija kwa wanachama wa TALFA.

x) Ufuatiliaji na utekelezaji wa masuala yote ya Kikundi;

## IBARA YA 3: AINA, SIFA, HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA

### 1) Aina ya Wanachama;

Kuna wanakikundi wa aina tatu kama ifuatavyo;

a) **Wanachama waanzilishi**

Ambao watakuwa ni wale wanachama wote waliojiunga wakati wa kuanzishwa kwa umoja;

b) **Wanachama wapya**

Ambao watakaojiunga baada ya kikundi hiki kuanzishwa na baada ya kutimiza masharti ya kujiunga na kikundi;

c) **Wanachama wa heshima**

Ambao ni watu wanaojitoa kuchangia kwa hali na mali ili umoja uendelee.

### 2) Sifa za kujiunga na Umoja

Mtu yeyote anaye hitaji kujiunga na **Umoja** anatakiwa kutimiza masharti yafuatayo;

a) Awe ni mtanzania;

b) Awe mwenye akili timamu;

c) Awe anafuga kuku wanaozalisha mayai;

d) Asiwe na deni katika kikundi;

e) Awe na umri usiopungua miaka Kumi na nane(18);

f) Awe ni mtu anayekubaliana na taratibu, kanuni na katiba za Kikundi;

TALFA

g) Awe mwadilifu, mwaminifu, mkweli na sio mpenda majungu;

h) Awe ametoa mchango wa kiingilio na mchango wa mwezi;

i) Awe ni mtu wa kujituma.

**3) Haki, Wajibu na Maadili ya Mwanachama**

a) **Haki za Mwanachama**

Wanakikundi wote watakuwa na haki zifuatazo:

i. Haki ya kuchagua, kuchaguliwa au kuteuliwa katika uongozi;

ii. Kuwa na uhuru wa kutoa mawazo na maoni ndani ya vikao halali vya Kikundi na hata kutoa ushauri kwa uongozi wa Kikundi;

iii. Kushiriki katika shughuli zote zinazohusiana na Kikundi;

iv. Kufarijiwa na wanachama wakati wa shida kwa mfano msiba, ugonjwa na kwenye changamoto nyingine za maisha zinazotambuliwa na Kikundi;

v. Haki ya kujitetea au kutoa maelezo mbele ya wanachama kuhusiana na mashauri/malalamiko dhidi yake kabla ya kuchukuliwa hatua zozote za kinidhamu juu yake;

vi. Kuheshimiwa na kutathiminiwa;

vii. Kupata taarifa zote muhimu za Kikundi kwa mujibu wa taratibu zilizopitishwa na mkutano mkuu

viii. Kuwa na haki sawa na mwanakikundi mwingine.

TALFA

b) **Wajibu wa Mwanachama**

Mwanachama anawajibika kutekeleza yafuatayo:

i. Kuhudhuria vikao vyote halali vya Umoja wa kikundi hiki;
ii. Kutii na kuheshimu maamuzi ya wanachama na viongozi wa Kikundi;
iii. Kulinda na kutetea katiba ya Kikundi hiki na maamuzi mbalimbali ya vikao.
iv. Kulipa ada, madeni, na michango yote kwa wakati, kama ilivyo kubaliwa na wanachama na kwa mujibu wa taratibu na kanuni halali kama zilivyo fafanuliwa ndani ya katiba hii.
**v.** Kushiriki kikamilifu katika shughuli za Umoja kama itakavyo amuliwa na kukubaliwa na wanachama
**vi.** Kutunza siri za Kikundi;
**vii.** Kuwa mwaminifu ndani na nje ya kikundi;
**viii.** Kujifunza na kujielimisha katika shughuli za kikundi.

**c) Kukoma au kuacha Uanachama**

Mwanachama atakoma au kuacha uanachama ikiwa moja kati yafuatayo yatatokea;

i. Kifo;
**ii.** Kurukwa na akili au kupatwa na uchizi wa kudumu;
iii. Ameamua mwenyewe kujitoa kwenye umoja (kujiuzulu mwenyewe);

iv. Atashindwa kulipa ada ya mwezi, kwa muda miezi mitatu mfululizo pasipo sababu yeyote ya msingi iliyo kubaliwa na wanchama;

v. Kutohudhuria vikao vitatu (3) mfululizo vya Kikundi bila taarifa au sababu yeyote ya msingi;

vi. Kushindwa kwa makusudi kutoa ushirikiano katika shughuli mbali mbali za Umoja, kama vile kuchangia michango katika matukio mbalimbali ya misiba, majanga au sherehe mabali mbali za wanachama kama ilivyo ainishwa kwenye katiba na kanuni;

vii. Kufukuzwa uanachamana mkutano mkuu halali wa Kikundi kutokana na Kutokuwa mwaminifu katika Kikundi, Kutoa rushwa au kupokea rushwa kwa viongozi wa Kikundi kwa nia ya kupata upendeleo, Utovu wa nidhamu pamoja na kutokuwa mtii katika Kikundi, Kushindwa kulipa michango katika muda ulioruhusiwa na Kikundi bila ya kuwa na sababu zinazokubalika na Kamati ya Utendaji;

viii. Kufanya kazi binafsi kwa kutumia jina la kikundi bila kuwa na taarifa rasmi;

ix. Mwanachama ambaye uanachama wake utakoma kwa kuzingatia katiba hii ibara ya 3 (c) (i) na (ii), Mweka hazina wa kikundi atapiga hesabu ya fedha iliyopo, jumla yake itagawanywa kwa idadi ya wanachama, kujua kila mmoja angestahili gawiwo la kiasi gani, na warithi wa mhusika aliye fariki au kuugua ugonjwa wa akili wa kudumu watapewa asilimia hamsini (50%) ya gawiwo ambalo mwanachama angeastahili kupata;

**x.** Iwapo mwachama ataacha uanachama kwa kujiuzulu kwa hiari au kufukuzwa uanachama atarudishiwa kiasi cha asilimia Ishirini (20%) cha ada au kiingilio alicholipa chamani;

**xi.** Kupoteza sifa za kuwa mwanachama;

**xii.** Aidha, mwanachama aliyefukuzwa au kujiuzulu anaweza kupata sifa za kuwa mwanachama endapo atatimiza masharti, kanuni na taratibu zilizowekwa na mkutano mkuu wa mwaka utaridhia kwa mujibu wa katiba hii.

**IBARA YA 4: FEDHA NA MALI ZA UMOJA**

**a) Vyanzo vya Mapato ya Umoja**

i. Kiingilio;

ii. Michango ya Hiari ya wana-Kikundi, Wahisani, Jamaa na Marafiki;

iii. Ada za kila mwezi;

iv. Hisa;

v. Ushuru wa zo la Alizeti unaoweza kutozwa kwa mujibu wa masharti ya katiba hii na kanuni zake;

**vi.** Faini zitokanazo na adhabu mbalimbali kama zilivyoainishwa kwenye kanuni za Kikundi;

**vii.** Zawadi, na misaada itokanayo na Wafadhili;

**viii.** Akiba za fedha za chama zilizowekwa;

**ix.** Malimbikizo ya ziada;

TALFA

**x.** Faida itakayopatikana kutoka kwenye shughuli ya uzalishaji mali zitakazobuniwa na kuidhinishwa na wanachama;

xi. Mikopo yenye Riba nafuu toka taasisi za fedha.

**b) Taratibu za Fedha ya Chama**

i. Fedha zote za Umoja zitahifadhiwa Benki katika akaunti itayokuwa na jina la Chama;

ii. Malipo yataidhinishwa na Mwenyekiti wakishauriana na Katibu;

iii. Watakaohusika kutoa fedha Benki watakuwa wanachama wanne(4) ambapo kundi A litakuwa na Viongozi wakuu wawili(2); yaani Mwenyekiti na Mtunza Hazina na Kundi B litakuwa na wanachama wawili (2) watakaoteuliwa na wanachama wote katika mkutano mkuu wa Mwaka wa Chama

iv. Wakati wa kutoa fedha Benkoi ni **lazima watia saini waanzie watatu na kila kundi litoe mtia saini angalau mmoja kuweka sahihi zao ili pesa ziweze kutolewa Benki;**

**c) Watia Saini Benki**

i. Watakaohusika kutoa fedha Benki watakuwa wanachama wanne(4) ambapo kundi A litakuwa na Viongozi wakuu wawili(2); yaani Mwenyekiti na Mtunza Hazina na Kundi B litakuwa na wanachama wawili (2) watakaoteuliwa na wanachama katika mkutano mkuu wa Mwaka wa Chama

ii. Wakati wa kutoa fedha Benkoi ni **lazima watia saini waanzie watatu na kila kundi litoe mtia saini angalau**

**mmoja kuweka sahihi zao ili pesa ziweze kutolewa Benki;**

**d) Mali za Umoja**

Huduma hiii iitakuwa na mali inayohamishika na isiyohamishika ambayo itatunzwa na kuwekwa chini ya Bodi ya wadhamini;

**e) Taarifa ya Fedha ya mwaka**

i. Kutaandaliwa na kuwasilishwa taarifa ya fedha ya mwaka katika mkutano mkuu wa mwaka;

ii. Aidha katika taarifa hiyo ya fedha, kutakuwepo na taarifa ya utekelezaji kadri itakavyokuwa imeamriwa na mkutano mkuu.

**f) Ukaguzi wa Mahesabu**

i. Vitabu na taarifa za mahesabu ya chama vitatunzwa na mhazini na vitabu hivyo vitakaguliwa na kamati Tendaji kila baada ya miezi mitatu (3);

ii. Ripoti ya ukaguzi ya mwisho wa mwaka itawasilishwa katika mkutano mkuu wa wanachama wote;

iii. Mahesabu ya chama yaliyokaguliwa yatakuwa bayana na yataweza kuangaliwa na mwanachama yeyote;

iv. Ukaguzi wa mahesabu ya chama pia unaweza kufanywa na mkaguzi wa mahesabu mwenye utaalamu na aliyesajiliwa na bodi mahesabu na wakaguzi wa mahesabu wa Tanzania. Gharama za ukaguzi zitalipwa na mfuko wa chama.

TALA

## IBARA YA 5: UONGOZI WA UMOJA

### 1) Uongozi wa Umoja

Kutakuwa na Uongozi wa Umoja ambao ni;

a) Mwenyekiti;
b) Makamu Mwenyekiti;
c) Katibu Mkuu;
d) Katibu Mkuu Msaidizi;
e) Mweka Hazina;
f) Mweka Hazina Msaidizi;
g) Kamati tendaji;
h) Kamati ndogo ya nidhamu;
i) Kamati ndogo ya fedha.

### 2) Sifa za Viongozi wa Kikundi

Ili mwachama aweze kuchaguliwa kuwa kiongozi ni lazima awe na sifa zifuatazo:-

a) Awe mwanachama hai wa Umoja;
**b)** Awe na akili timamu;
**c)** Awe amechangia michango yote ya Kikundi;
**d)** Awe ni muhudhuriaji mzuri wa mikutano ya Kikundi;
**e)** Asiwe mbadhirifu au kuwa na kashfa ya fedha au mali za umma;
**f)** Asiwe na rekodi ya kifungo cha jela kwa makosa ya jinai;
**g)** Awe amejiunga na kikundi sio chini ya miezi 12;
**h)** Awe ni mtu mwenye moyo wa kujituma na kujitolea kwenye shughuli za kila siku za Umoja;

TALFA

**i)** Asiwe mtu wa kutumia madaraka yake kwa kujinufaisha yeye mwenyewe;

**j)** Asitoe uamuzi wowote wala kutenda jambo lolote kinyume na kaitba ya kikundi.

**3) Kazi za Viongozi**

**a) Mwenyekiti**

Mwenyekiti wa Kikundi atakuwa na majukumu yafuatayo;

i. Awe na umri usiopungua miaka thelathini a tano (35) na atakuwa ndiye msemaji mkuu wa Umoja;
ii. Kuwa muongozaji mkuu wa mikutano na vikao vyote vya Kikundi;
iii. Kutoa uamuzi wa mwisho kwa jambo lisilohitaji kupigiwa kura;
iv. Kutoa taarifa za maendeleo ya Umoja kwenye mkutano mkuu wa wanachama wote;
v. Atawakilisha Umoja katika majukumu na mikutano mbalimbali itakayofanyika nje ya Umoja (kitaifa na kimataifa);
vi. Ataidhinisha fedha za matumizi mbalimbali ya Umoja baada ya kuruhusiwa na kamati tendaji;
vii. Msuluhishaji, mtatuzi, na mshauri mkuu wa njia bora za kutatua migogoro inayojitokeza ndani ya Kikundi**;**
viii. Atakuwa na kura ya uamuzi, iwapo kura za wanachama wanaoafiki na wasioafiki zitalingana/fungana.

TALA

b) **Makamu Mwenyekiti**

Makamu Mwenyekiti atakuwa na majukumu yafuatayo;

i. Awe na umri usiopungua miaka thelathini a tano (35) na atamsaidia Mwenyekiti katika majukumu yake kama yalivyo ainishwa hapo juu, wakati Mwenyekiti hayupo au iwapo Mwenyekiti atamwelekeza kufanya hivyo;
ii. Atatekeleza majukumu yote atakayo pangiwa na kamati tendaji au mkutano mkuu wa Umoja;
iii. Atashirikiana na Mwenyekiti na Mtunza hazina kufuatilia na kukusanya madeni yote kutoka kwa wanachama.

**c) Katibu**

Katibu wa kikundi atakuwa na majukumu yafuatayo;

i. Awe na umri usiopungua miaka kumi na nane (18) na atakuwa mtendaji mkuu wa shughuli za kila siku za umoja;
ii. Ataratibu na kuandaa vikao na mikutano yote ya Kikundi kwa kushirikiana na Mwenyekiti;
iii. Ataandaa na kutunza taarifa za kumbukumbu zote za Kikundi, zikiwemo Muhtasari (minutes) za vikao vyote vya kikundi, fomu za maombi ya uanachama, katiba ya kikundi na orodha ya mali za Kikundi;
iv. Kudhibiti, kutunza siri na nyaraka mbalimbali za Kikundi;
v. Kudhibiti na kutunza mali za Kikundi;
vi. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za maandishi kila zinapotakiwa

vii. Kufanya kazi nyingine atakazo pangiwa na Kikundi hiki.

**g) Katibu Msaidizi**

Awe na umri usiopungua miaka kumi na nane (18) na atafanya na kutekeleza majukumu yote ya katibu, pale ambapo katibu atakuwa na dharura au atamwelekeza kufanya hivyo.

**h) Mweka Hazina**

**i.** Awe na umri usiopungua miaka ishirini (20)

**ii.** Atahusika katika utunzaji wa fedha zote za Kikundi;

iii. Atakuwa mwenye mamlaka ya kipekee ya kukusanya fedha zote za kikundi, na kufanya malinganisho ya fedha iliyopokelewa na iliyolipwa;

**iv.** Atakuwa mwenye mamlaka ya kipekee ya kuhidhinisha malipo yote ya fedha kwa shughuli mbalimbali za umoja wa Kikundi hiki;

**v.** Muandaaji na mdhibiti mkuu wa bajeti ya Umoja;

**vi.** Kuandaa na kutoa taarifa ya fedha (Mapato na Matumizi) ya Kikundi kwenye Mikutano mbalimbali ya Umoja huu;

**vii.** Kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya kikundi na mizania kila baada ya miezi mitatu (3);

**viii.** Kuonyesha Ankara za Benki (Current Bank Statement) katika vikao mbalimbali vya Kikundi na kwenye Mkutano Mkuu pale itakapohitajika;

**ix.** Atashirikiana na Mwenyekiti kukabidhi michango inayotolewa kama misaada kwa wana kikundi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Umoja;

**x.** Kutayarisha orodha ya wadaiwa kila mwezi na kuwakilisha kwenye vikao vya kila mwezi vya Kikundi ambavyo vitatoa maamuzi juu ya hatua stahiki za kufuatwa kwa wanachama waliochelewesha michango yao zaidi ya miezi mitatu;

**xi.** Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na wanachama.

**iii. Mweka Hazina Msaidizi**

**i.** Awe na umri usiopungua miaka ishirini (20)

ii. Atamsaidia majukumu Mtunza Hazina mkuu;

iii. Atakaimu nafasi ya Mtunza hazina mkuu pindi Mtunza Hazina Mkuu anapokuwa hayupo kwa sababu mbalimbali.

**iv. Kamati tendaji**

Kutakuwa na Kamati tendaji itakayoundwa na WAJUMBE KUMI (10) ambapo SITA (6) ambao ni Viongozi na wajumbe WANNE (4) watakao pendekezwa na kuthibitishwa kwenye mkutano mkuu wa wanachama kutoka miongoni mwa wanachama, baada ya mapendekezo ya majina ya wajumbe, kama majina yaliyopendekezwa yatazidi manne, basi majina hayo yatapigiwa kura na kuwapata wajumbe wanne watakao kuwa miongoni mwa wajumbe wa kamati tendaji ya Umoja ambapo kamati hii itadumu kwa miaka miwili (2) na kutakuwa na uchaguzi wa kuwachagua wajumbe wapya wa kamati. **KAMATI hiyo itakuwa na majukumu yafuatayo;**

i. Kuandaa miongozo mbalimbali kwa mujibu wa katiba ya chama ili iweze kutumika katika kudumisha nidhamu

TALFA

kwa wanachama wa kikundi na itatumika mara tu itakapopitishwa na makao makuu.

ii. Kusimamia shughuli za kila siku za Umoja wa kikundi hiki;

iii. Kutoa taarifa ya mwaka juu ya shughuli za Kikundi(mafanikio na changamoto) kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa Umoja;

iv. Kubuni, kuendeleza na kusimamia shughuli mbalimbali za maendeleo ya Kikundi hiki;

v. Kupokea na kujadili malalamiko mbalimbali ya mwanachama;

vi. Itajadili na kupendekeza adhabu inayostahili kwa mwanachama aliye kiuka au kwenda kinyume na taratibu na kanuni za Umoja au kufanya kosa lolote la utovu wa nidhamu;

vii. Kuandaa bajeti ya mwaka ya Umoja;

viii. Kupokea maombi ya wanachama wapya wanaoonesha nia ya kujiunga na Umoja;

ix. Itajadili na kuidhinisha au kukataa maombi ya mkopo wa mwanachama na kutoa sababu za kukataa maombi ya mkopo kwa mwanachama husika.

**v. Kamati ndogo ya nidhamu**

Kutakuwa na kamati ndogo ya nidhamu na itakuwa na Wajumbe Watatu (3) ambao watachaguliwa kwenye Mkutano mkuu wa Uchaguzi.Kamati hiyo itakuwa na majukumu yafuatayo;

i. Kuandaa miongozo mbalimbali inayotumika katika kudumisha nidhamu kwa wanachama wa kikundi na itatumika mara tu itakapopitishwa na mkutano mkuu;

ii. Kutatua migogoro na kutoelewana pindi kunapojitokeza miongoni mwa wanachama au baina ya wanachama na uongozi;

iii. Kushauri na kupendekeza iwapo mwanachama amepoteza sifa za kuwa uanchama na hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake;

iv. Kazi na shughuli yoyote itakayoamriwa na mkutano mkuu kwa maslahi ya kikundi na kwa mujibu wa katiba hii.

**vi. Kamati ndogo ya Mikopo na Fedha**

Kutakuwa na kamati ndogo ya Fedha ambayo itakuwa na wajumbe watatu na watachaguliwa katika mkutano mkuu wa uchaguzi wa kikundi.Kamati hiyo itakuwa na majukumu yafuatayo;

i. Kujadili masuala ya fedha, ikiwepo bajeti, kufanya mapitio na kuwasilisha ushauri na mapendekezo kwenye kamati tendaji ili yafanyiwe kazi;
ii. Kupokea na kujadili maombi ya wanachama wanaohitaji kupewa mikopo midogomidogo toka chamani;
iii. Kubuni vyanzo vya fedha vya kikundi;

TALFA

iv. Kupanga mipangilio ya kuongeza kipato kwa kikundi na wanachama kwa ujumla;

v. Kutafuta wafadhili na wahisani wa Kikundi;

vi. Kazi na shughuli zingine kama itakavyokuwa imeamriwa na mkutano mkuu wa kikundi.

4) **Ukomo Wa Uongozi**

Ukomo kiongozi utakuwa kama ifutatvyo;

**i.** Anapofariki;

**ii.** kuugua ugonjwa wa akili wa kudumu

**iii.** kuhukumiwa na mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania adhabu ya kifungo cha jela kwa makosa ya jinai na nafasi yake ya uongozi pia itakoma;

**iv.** Pia viongozi/Kiongozi anaweza kuondolewa madarakani kabla ya muda wake iwapo ¾ ya wanakikundi watapiga kura ya kutokuwa na imani na kiongozi au viongozi hao. Hili litafanyika baada ya wanachama kuorodhesha majina yao na tuhuma zinazomhusu kiongozi au viongozi husika;

**v.** Kiongozi yeyote anaweza kuondolewa madarakani kabla muda wake wa uongozi kuisha iwapo uanachama wake utakoma kama ilivyoelezwa kwenye katiba hii;

**vi.** Nafasi ya uongozi ikiachwa wazi kwa sababu yeyote ile, kamati ya utendaji itajaza nafasi hiyo, kwa kupendekeza mwanachama atakaye weza kukaimu nafasi iliyoachwa wazi na uchaguzi wa kuziba nafasi hiyo utafanywa na wanachama katika mkutano wa wanachama wote katika kipindi kisichozidi siku Tisini (90)

TALA

**5) Muda wa kiongozi kukaa madarakani**

Muda wa Kiongozi kukaa madarakani ni miaka Mitatu (3) kwa muhula mmoja na ataruhusiwa kuchaguliwa tena kwa muhula wa pili katika nafasi yake ya uongozi.

**IBARA YA 6: UCHAGUZI**

**1) Uchaguzi wa Viongozi wa Umoja**

**a)** Kutakuwa na kamati maalumu ya Uchaguzi ambao itasimamia uchaguzi husika pamoja na kuhesabu kura;

**b)** Uchaguzi wa viongozi utafanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni za Umoja;

c) Uchaguzi wa viongozi utafanywa kwa kupiga kura ya siri;

d) Upigaji wa kura utakuwa ni wakutumia karatasi maalumu zilizoandaliwa na kamati ya uchaguzi itakayoundwa na kamati tendaji;

e) Viongozi wa Umoja watachaguliwa na wanachama waliohudhuria kwenye mkutano mkuu tu.

**2) Taratibu za Uchaguzi kwa Viongozi wa Kikundi**

a) Viongozi na Kamati zote zilizoanishwa kwenye katiba zitachaguliwa na wanachama hai tu katika mkutano mkuu. Aidha, ni wanachama wa kawaida wenye sifa za uanachama wa kikundi hiki ndio watakaogombea uongozi wa chama.

b) Mwanachama atapaswa kujaza fomu maalum kwa ajili ya kuomba kugombea nafasi anayohitaji.

c) Baada ya hapo jina la mwombaji litapelekwa kwenye mkutano mkuu wa uchaguzi kwa ajili ya kupigiwa kura za siri, atakeyapata kura nyingi zaidi ya mgombea mwenzake ndiye atakuwa mshindi wa nafasi hiyo.

TALFA

d) Katika mkutano wa uchaguzi theluthi mbili **2/3** ya wanachama wana haki ya kuchagua viongozi na Kamati Tendaji.

e) Uongozi itakaochaguliwa na itakaa madarakani kwa muda wa miaka mitano (5).

f) Kiongozi na na Mjumbe wa Kamati tendaji aliyemaliza muda wake anaweza kugombea tena baada ya muda wake wa uongozi kumalizika kwa kipindi kingine cha pili

g) Baada ya vipindi viwili kuisha hata kama atakuwa na sifa hataruhiwa mpaka apumzike miaka mitatu (3) ila anaweza kuruhusiwa kugombea nafasi nyingine kwa kubadilisha uongozi baada ya muda wake wa uongozi kumalizika.

h) Viongozi wa kuchaguliwa watakuwa ni mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Katibu Mkuu Msaidizi, Mweka hazina , Mweka Hazina Msaidizi na Kamati Tendaji na kamati nyinginezo.

**IBARA YA 7: MIKUTANO YA UMOJA**

1) **Aina ya Mikutano**

Kutakuwa na Mikutano ya aina Nne:

a) Mkutano mkuu wa Mwaka;
b) Mkutano Mkuu wa Mwezi (Mkutano wa kawaida);
c) Mkutano Mkuu Maalumu (MKUTANO WA DHARURA);
d) Vikao vya kamati tendaji.

**2) Taratibu na Majukumu ya mikutano**

**a) Mkutano Mkuu wa Mwaka**

**i.** Mkutano mkuu wa mwaka wa kikundi utafanyika mara moja kwa mwaka. Mkutano huu wa mwaka ndio chombo

TALFA

chenye mamlaka ya mwisho katika uamuzi na usimamizi wa shughuli zote za Baraza;

ii. Taarifa kwa maandishi kuhusu tarehe ya mkutano mkuu na itasambazwa kwa wanachama wote kwa siku zisizopungua ishirini na moja (21) kabla ya kikao ikiambatana na taarifa ya mwaka ya mahesabu na agenda za kikao;

iii. Mahudhurio ya mkutano mkuu yasipungue theluthi mbili (2/3) ya wanachama wote;

iv. Idadi isipotimia mwenyekiti ataahirisha mkutano na kupanga siku nyingine ya kufanya mkutano na idadi yoyote ya wanachama watakao jitokeza katika mkutano huu itafanya mkutano mkuu kuwa halali;

v. **Mkutano huu** utachagua viongozi wapya iwapo muda wa kufanya hivyo umefika;

vi. Utapitia na kujadili taarifa za Kikundi za mwaka ikiwamo kuthibitisha, kurekebisha au kutengua taarifa za kamati tendaji;

vii. Utapokea na kujadili hesabu za mwaka (Annual Financial Statements), muhtasari wa taarifa za ukaguzi na taarifa nyinginezo kama zilivyoainishwa kwenye katiba hii;

viii. Kupokea na kujadili makisio ya bajeti ya kikundi kwa mwaka unaofuata;

ix. Kujadili namna ya kugawana ziada kama ipo kwa kuzingatia sheria, kanuni na masharti ya kikundi;

x. Kujadili mapendekezo ya miradi na mipango mikakati ya Umoja na kutoa maamuzi;

xi. Kujadili na kufanya marekebisho ya katiba ikiwa kutaonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo;

TALA

xii. Kupitisha maamuzi ya mwisho juu ya jambo lolote ambalo lilikuwa bado halijapatiwa ufumbuzi katika vyombo vya maamuzi;

**b) Mkutano Mkuu wa Mwezi (Mkutano wa kawaida)**

Kutakuwepo na mkutano mkuu wa wanachama wote ambao utakuwa ukifanyika angalau mara moja kwa mwezi, wajumbe wa mkutano huu wasipungue 1/3 ya wanachama wote. Ambapo **mambo yafuatayo yatajadiliwa katika mkutano mkuu wa kawaida**:

i. Kuthibitisha muhtasari wa mkutano uliopita na yatokanayo;
ii. Kupokea na Kujadili taarifa mbali mbali za Maendeleo ya Kikundi na utekelezaji wake;
iii. Kuthibitisha kuingizwa au kufukuzwa kwa mwanachama;
iv. Kuidhinisha na kukusanya michango mbalimbali ya Kikundi kama vile; Ada, faini, kiingilio, na marejesho ya mikopo

**c) Mkutano Mkuu Maalumu ( mkutano wa dharura)**

**i.** Mkutano mkuu maalumu utaitishwa kwa dharura;

**ii.** Taarifa ya Mkutano Mkuu maalumu pamoja na agenda ya kikao zitumwe kwa njia ya posta au barua pepe kwa wanachama siku zisizopungua 14 kabla ya tarehe ya mkutano

**iii.** Mkutano mkuu maalum utafanyika wakati wowote iwapo utaitishwa na viongozi, au kwa maombi ya maandishi ya wanachama wasiopungua theluthi moja (1/3);

TALA

iv. Mkutano mkuu maalum ukiombwa na wanachama, maombi ni lazima yataje sababu za kutaka mkutano huo ufanyike, na waombaji lazima waweke sahihi zao na wapeleke maombi hayo kwa mwenyekiti wa Kikundi;

**d) Vikao va Kamati Tendaji**

Vikao vya kamti tendaji vitafanyika mara moja kwa wiki ambapo ili kikao hiki kiwe halali ni lazima mahudhurio ya wajumbe wake yasipungue Nusu (1/2) ya Wajumbe wote wa Kamati tendaji.**Agenda za vikao vya kamati tendaji zitakuwa;**

i. Kupokea na kujadili muhtasari wa yatokanayo na kikao kilichopita.

ii. Kupanga na kuandaa agenda za mikutano mbalimbali ya Chama.

iii. Kupokea maombi ya watu wanaomba kujiunga na chama na kuyajadili.

iv. Kutayarisha kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za Chama kama zilivyopendekezwa na mkutano wa wanachama wote

v. Kutoa maamuzi ya mwisho juu ya jambo lolote ambalo kamati ina madaraka ya kufanya hivyo kwa mujibu wa katiba.

**e) Vikao vya Kamati ndogo ya Nidhamu**

Vikao vya Kamati ndogo ya Nidhamu vitakuwa na kazi zifuatazo;

i. **Ita**hakikisha usahihi wa kumbukumbu za fedha na mali za chama;

ii. Kujadili na Kushughulikia nidhamu ya viongozi na wanachama;

TALA

iii. Kujadili usimamizi wa nidhamu ya kikundi pamoja na kulinda katiba ya kikundi isivunjike;

iv. Kupokea taarifa ya maadili ya wanachama;

v. Kupendekeza kwa mkutano mkuu wa wanachama hatua za nidhamu kwa wanachama;

vi. Kutekeleza kazi na majukumu kama itakavyoamriwa na mkutano mkuu.

**f) Vikao vya kamati ndogo ya Mikopo na Fedha**

Vikao vya Kamati ndogo ya Fedha vitakuwa nna kazi zifuatazo

i. Kupendekeza na kupanga bei za bidhaa ambazo umoja watakuwa wanazalisha kwa kuangalia hali ya uzalishaji na soko husika;

ii. Kupanga bajeti ya matumizi katika jambo lolote litakalo hitaji fedha na kuwasilisha sehemu husika na kuandaa na kutoa taarifa katika mkutano mkuu

iii. Kujadili juu ya miradi ya kujiongezea kipato kwa wanakikundi na kikundi kwa ujumla;

iv. Kujadili maombi ya wanachama wanaohitaji mikopo toka chamani;

v. Kupokea na kujadili mapendekezo ya kuwa na vyanzo vya mapato na kutoa ushauri wa kuwa na vyanzo vipya vya mapato;

vi. Kupanga mipango mbalimbali ya kiuchumi na kuiwasilisha kwenye kamati tendaji;

TALFA

vii. Kufuatilia na kusihauri kamati tendaji kufanya mafunzo ya kuwajengea uwezo wanakikundi na jamii kwa ujumla juu ya masuala ya ujasiriamali;

viii. Kufanya mapitio ya miradi na mipango ya kikundi na wanakikundi na kushauri;

ix. Kutekeleza kazi na shughuli iliyoamriwa na mkutano mkuu.

**3) Taarifa za Mkutano**

**a)** Kamati tendaji itatoa taarifa ya kila mkutano kwa maandishi kwa kila mjumbe katika muda usiopungua siku theleathini (30) ikieleza mahali, siku na saa ya mkutano unakusudiwa kufanyika na mambo yatakayojadiliwa na mkutano**;**

b) Taarifa ya mkutano itaambatanishwa na nyaraka au kumbukumbu muhimu zitakazo tumika katika mkutano huo ;

c) Kila mkutano ni lazima utmize Akid ya theluthi mbili (2/3) ya wanachama au wajumbe wote wa mkutano husika ;

**IBARA YA 8: TARATIBU ZA KUTATUA MIGOGORO**

**a)** Umoja huu utakuwa na nguvu na uwezo wa kushtaki na kushtakiwa katika mahakama yeyote Tanzania;

**b)** Na endapo kutatokea mgogoro wowote katika umoja huu, basi utashughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi na kamati ya nidhamu itakayoundwa na kamati tendaji;

**c)** Endapo kamati ya nidhamu itashindwa kupatia ufumbuzi mgogoro huu, basi mgogoro utapelekwa kwenye Kamati tendaji ya Chama;

TALA

**d)** Endapo Kamati Tendaji itashindwa kupatia ufumbuzi mgogoro huo, basi mgogoro huo utapelekwa kwenye mkutano wa wanachama wote au mkutano wa dharura ulioitishwa maalumu kwaajili ya kutatua mgogoro husika;

**e)** Iwapo mgogoro utashindikana kupatiwa ufumbuzi na mkutano maalumu wa kutatua mgogoro, basi mgogoro huu utapelekwa kwa viongozi wa serikali katika ngazi ya mtaa ofisi ya kikundi ilipo;

**f)** Huko pia muafaka usipopatikana basi mgogoro huo utapelekwa kwa msajili wa vyama na maamuzi yake na;

**g)** Endapo Msajili wa vyama atashindwa kupatia ufumbuzi mgogoro huu, basi mgogoro utapelekwa Mahakamani.

**IBARA YA 9: MABADILIKO YA KATIBA**

Bila kuathiri vifungu vingine vya katiba, marekebisho ya katiba hii yatafanyika kwa kuzingatia yafuatayo:

**a)** Katiba hii itafanyiwa marekebisho iwapo wanachama wataona kuna umuhimu wa kufanya hivyo, na kutoa mapendekezo yanayoonesha vipengele vinavyo pendekezwa kufanyiwa marekebisho (mapendekezo hayo ni lazima yatolewe kwa maandishi na kupelekwa kwa kamati tendaji);

**b)** Pendekezo lolote la kubadilisha katiba ni lazima lipitishwe na theluthi mbili (2/3) ya wanachama wote.

TALFA

**c)** Marekebisho ya katiba yatakuwa halali iwapo yatapitishwa na mkutano mkuu wa kikundi, au mkutano maalumu utakao itishwa na viongozi kwaajili ya kufanya marekebisho ya katiba.

**IBARA YA 10: KUVUNJIKA KWA KIKUNDI**

a) Sio lengo la Katiba hii wala la wanachama wa Umoja kuvunja Umoja huu wa kijamii siku moja, LAKINI ikitokea Kikundi hiki kimevunjika kwa sababu yoyote ya msingi, zikiwemo zile zinazotokana na:-

i. Maombi ya wanachama wasiopungua 3/4 ya wanachama wote wanaotaka kikundi kivunjike;
ii. Kupungua kwa wanachama mpaka kufikia chini ya wanachama 10;
iii. Amri ya msajili wa vyama vya kiraia kwa kuzingatia misingi ya sheria na kanuni za vyama vya kiraia, au amri ya mahakama ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

b) Baada ya Umoja Kuvunjika, mambo yafuatayo yatazingatiwa kwenye mali na fedha za kikundi:

i. Kulipa madeni yote ya Umoja kama yatakuwepo aidha kwa hundi au kwa pesa taslimu;

ii. Kugawa kwa wenye hisa endapo kutakuwepo na mfuko wa akiba na mikopo;

TALA

iii. Mali za kudumu za kikundi zilizopo zitauzwa, na fedha zote zitakazopatikana zitachanganywa na pesa za Umoja zilizopo kwa wakati huo, na kila mwanachama atagawiwa kiasi cha pesa, kulingana na kiasi cha pesa (michango) alicho changia katika kipindi chote cha uhai wa Umoja.

**IBARA YA 11: MUHURI AU LAKIRI YA HUDUMA**

a) Kutakuwa na muhuri au lakiri ya huduma kwa jina la Umoja ambao utakuwa ukitumika kwenye nyaraka zote zinazohusiana na Umoja ;

b) Muhuri huo utakuwa ukitunzwa katika ofisi ya huduma na mtu ambaye atakuwa na wajibu wa kufanya hivyo kwa mujibu wa katiba

**IBARA YA 12: TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA:**

Katiba hii imeaanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 26/9/2017 mara baada ya kuidhinishwa na kupitishwa na Msajili wa vyama.

TALFA